



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



Kumb.Na. AB.53/172/01/38

15 Julai, 2024

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela amepokea kibali cha Ajira Mpya kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuitia barua yenyewe **Kumb. Na. FA. 97/288/01/09 ya tarehe 25 Juni, 2024.** Hivyo anakaribisha maombi ya Kazi kwa Watanzania wote wenye Sifa za kujaza nafasi ifuatayo:-

1.0 MTENDAJI WA MTAATARAJA LA III – NAFASI THELATHINI (30).

1.1 MAJUKUMU

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji mkuu wa serikali ya Mtaa
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Mtaa
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa mipango ya maendeleo ya Mtaa
- iv. Kusimamia mapato ya Halmashauri katika Mtaa
- v. Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Mtaa
- vi. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
- vii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali;
- viii. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika Mtaa
- ix. Kuandaa na kutunza kumbukumbu zote na nyaraka za Mtaa;
- x. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika Mtaa
- xi. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- xii. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Mtaa; na
- xiii. Atawajibika kwa Mtendaji Mkuu wa Kata.
- xiv. Pamoja na kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri wako.

1.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Waombaji wanatakiwa wawe wenye Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Sita (Form Six) aliyehitimu astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B.**

2.0 MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;
- ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma**
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia Sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria / Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kaži husika.
- vi. "Testmonial", "Provisional Results", "Statement of results", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyaao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **28 Julai, 2024**.
- xii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPA
200 BR YA BUSWELU,
33282 BUSWELU,
S.L.P 735,
ILEMELA - MWANZA

- xiii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilioandikwa 'Recruitment Portal').
- xiv. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na;


Ummy M. Wayayu
**MKURUGENZI WA MANISPA
ILEMELA**

